

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA NISHATI



MAMLAKA YA UDHIBITI WA
HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI
(EWURA)



TANGAZO KWA UMMA

AGIZO KWA VIWANDA VYOTE NCHINI

Kwa mujibu wa Kifungu cha 8(1)(a) cha Sheria ya Umeme, Sura ya 131, na Kifungu cha 4(1) cha Kanuni za Shughuli za Uzalishaji, Usafirishaji na Usambazaji wa Umeme, Tangazo la Serikali Na.287 la mwaka 2019, kwa pamoja zinamtaka mtu yeyote anayezalisha umeme kwa matumizi binafsi kwa kiasi kinachozidi MegaWati moja (1MW) kuwa na leseni inayotolewa na EWURA.

Pia Kwa mujibu wa Kifungu cha 8(1)(h) cha Sheria ya Umeme, Sura ya 131 na Kanuni za Umeme (Huduma za Ufungaji wa Mifumo ya Umeme) za mwaka 2022, Kanuni ya 4 (1) kwa pamoja zinamtaka mtu yeyote anayefanya shughuli za ufungaji wa mifumo ya umeme Tanzania Bara kuwa na leseni ya umeme iliyotolewa na Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA). Ukiukwaji wa takwa hili ni kosa linaloadhibiwa kisheria.

Kwa Mukstadha huo, Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) inavitaka Viwanda vyote Tanzania Bara kutimiza matakwa ya kisheria yaliyoainishwa hapo juu kwa kuomba leseni na pia kuhakikisha mafundi umeme wote wanaofanya kazi viwandani mwao wanakuwa na leseni kabla ya tarehe 31/7/2023.

Imetolewa na:
Mkurugenzi Mkuu
EWURA